https://dspace.org/

# Teamasn2022: Uvumbuzi Wa Umajumui Upelekee Uvumbuzi Wa Maenreleo Katika Mambasa

**Mohamed, Karama**

**2022-11**
Gombo La Isimu Tumi Ni Kufuwata Sat I Za Majagina Wa Isimu
http://ir-library.kabianga.ac.ke/handle/123456789/507

Downloaded from a DSpace repository. https://dspace.org/

# TEAMASN2022: UVUMBUZI WA UMAJUMUI UPELEKEE UVUMBUZI WA MAENRELEO KATIKA MAMBASA

Pʰongezi zimwenree Gavana Mpya wa Mambasa Mṯukufu Abdulswamad Shariff Nassir (ASN) kwa kuṯeuliwa kiyongozi wa jiji hili la kale. Tʰwashukuru ghaya Uchaguzi 2022 ulipita salama kwani Mungu alitikiya kabuli maombi yetʰu.

Makala haya yanaazimiya kuipongeza makhsusi Timu ilosimamiya kampeni za Gavana siyo kwa kufaulisha kuṯimiya maṯilaba yao bali kwingiza mbinu ya kiuvumbuzi kwenye kampeni za uchaguzi uliyopita hapo Mambasa. Pili, ni kupenḏekeza uvumbuzi wa mikakati ya kujumuisha wananchi woṯʰe wa Mambasa uwenrelee na piya katika mipangiliyo ya kimaenreleyo. Umajumui kwa maana ya kukutanisha fikira na matenro yoṯʰe ya wananchi wote mahali kumoja kufikiya lengo.

Mwanḏishi huyu kwamba ameshuhuḏiya kuṯokuwako New People’s Hotel, Bonreni, ṯangu ni kiṯaru na sasa ni jumba la kutambulika, iṯoshe kwamba jambo lililofanzwa na TEAMASN2022 (tʰwaipa jina hilo na soma ‘Timu’ sasa) ni jipya, la ubunifu, na la uvumbuzi katika miito ya au mbiyu za wanasiyasa.

Katika chʰaguzi za zama za ’70 na ’80 tulikuwa tukiyona miito ya Chʰupa Juu!, Ṯaa Juu!, Ṉḏovu Juu!, Ndizi Juu!, Siasa Si Chʰuki!, au Wanted In Parliament! Baaḏaye ikawa ni miito ya vyama va kisiyasa ya Chungwa Moja!, Kazi Iendelee! na mifano mengineyo. Wagombeyaji uṯeuzi walikuwa wakivutiya wapigaji kura wa jamii zoṯʰe kwa mbinu mbalimbali za magwaride mitʰaani, hafla za ṯaarabu, na magari ya matangazo. Mabango yalikuwa ya makaraṯasi meupe na baaḏaye kuwa ya rangirangi yaliyoengeza uvutiyo na ushawishi kwa wapigaji kura. Uchaguzi wa 2022 kampeni zake zilikuwa na msukumo mpya haswa kwenye mitanrao ya kijamii ambayo ilitumiwa kwa naṯija kubwa.

Upeo wa vinjari zangu wakaṯi Agosti 9 ilipokaribiya zilinipelekeya, mosi, kugunruwa na kushangwaza na kusṯaajabiya shani ambayo sijaiyonapo katika mabango yoṯʰe niliyoshuhuḏiya katika chʰaguzi zilizopita. Pili, maṯembezi yangu yalikitʰa kwenye barabara moja ṯu ya Old Malindi Road (au barabara ya Kisauni kama waiyitavo wenyeji wa huko). Nadhari yangu iliyangaziya kwenye mabango ya makaraṯasi yalobanrikwa kʰutani mwa maḏuka, majumba, mabamba na haṯa

makontena yaliyoko barabara hiyo. Tʰatʰu, sikutizama mavazi ya wagombeyaji uchaguzi wala pozi zao kwenye mabango hayo. Ne, niliyangaliya miito ṯu ya wagombeyaji wala si namna ilivoanḏikwa na kupachikwa pembe zipi za mabango hayo. Tʰano, huu ulikuwa mshawasha wa mṯembezi na wala si uṯafiṯi kwa maana ya uṯafiṯi.

Katika ukusanyaji wangu wa miito hiyo na uchanganuzi niloufanza ni: wa maneno machache (mawili matʰatʰu), ya kiSwahili na kiIngereza, ya kishawishi, ya kujikurubisha, ya kimafumbo, na ya kikawaida. Mifano ni: Maendeleo Mashinani, Mageuzi Halisi Mombasa, Kazi ni Sasa, Sauti ya Wanyonge, Mombasa One, The People's Project.

Lakini mabango ya Timu ninayoangaziya mimi haḏi nikasema ni uvyazi wa jambo jipya ni matumizi ya mbiyu inayotangazwa kwa lugha asiliya za jamii za Kenya mbali ya kiSwahili. Nilipata miito kwa mfano: Mtumishi wa Atu (kiMijikenra), Omurumikhi wa Bantu (kiLuhya), Muthukumi Wenyu (kiKamba), Jatij Jopiny (kiDholuo) yoṯʰe ina maana ya 'mtumwa wa watu' (servant of/for the people) au 'ulimwengu' kwa kiDholuo. Ltung'ani Lontung'ana (sic) (kiMaasai), Omonto bwa Abanto (ekeGusii), Chitab biik (Kipsigis), yenye maana ya Mtu wa Watu 'man of/for the people' ambayo piya ilitumika kama mojawapo ya mbiyu hizo; na Mutugati wa Adu (kiGikuyu) yenye maana 'Mchungaji wa Watu'. Fasiri za miito hiyo nilisaiḏiwa na wanafunzi wangu wazungumzaji wa lugha hizo katika Chama cha Kiswahili cha Kabianga (CHAKIKA). Mwito wa kiMaasai wanafunzi hawo walinambiya ulifaa uwe 'Oltung'ani Looltung'anak' kwa maana iliyorejelewa hapo awali.

Tuṯaona kuwa mbiyu za awali za wagombeyaji tulizotaja mwanzo ni za kuchukuliya kuwa wanaMambasa ni wananchi wasomi wanaojumuishwa kwa kiSwahili Sanifu na kiIngereza; wengi wa wananchi hawo ni wa ṯabaka la chini; na piya ni watʰu wanaoṯarajiya mabaḏiliko katika uṯeuzi wa mgombeya yoyoṯʰe nriposana kukawa na miito ya aina hiyo. Dhana hii hii ya haliya ilivo na maṯarajiyo piya niliishuhuḏiya kwenye mabango ya wagombeyaji huku kwetʰu Kabianga, Kericho. Kwa mfano: Chagua Roho Safi, Tsunami wa Maendeleo.

Timu piya walitumiya dhana hiyo hiyo ya 'kunyenyekeya' kwa kujiita 'mtumishi', 'mchungaji' na 'mtu' wa watʰu ambayo piya yaweza kufasiriwa kuwa 'mtʰu mwenye watʰu na si mpweke'. **Lakini, kwa mara ya kwanza** (msisitizo ni wetʰu), lugha za asili za watʰu wa bara, 'watʰu wageni' kama wanavoitʰwa na baadhi ya wenyeji wa Mambasa – sikubaliyani na dhana hiyo ya uwenyeji na ugeni kama nitakavofafanuwa – zimetumiwa na Timu hii katika kuwanaḏiya wapigaji kura kumpigiya mgombeyaji wao, ASN. Lugha za asili ya 'kibara' zishatumiwa kimaongezi katika chʰaguzi zilizopita, na haṯa huu, lakini kuwekwa kuwa miito kwenye mabango ni mkakati mpya ṯena haswa ikitiliwa maanani kuwa mgombeya uchaguzi wao si mwenye asili ya lugha yoyoṯʰe kati ya hizo za 'kibara'. Kwetʰu sisi hili ni jambo geni, lenye ubunifu mkubwa na tʰwaweza kuliita uvumbuzi.

Ni mkakati mpya, kwa sababu, kama nlivosema, haujawahi kutumiwa kama mbiyu kwenye mabango katika chʰaguzi zilizopita. Ni ubunifu mkubwa kwa sababu Timu

hii ilitiliya maanani wakaaji wa Mambasa 'Mpya' ambayo ni ya mchanganyiko wa jamii nyingi kuṯoka sehemu zoṯ$^{h}$e za Kenya; Kenya yoṯ$^{h}$e imo Mambasa sasa. Kwa hivo, badala ya kujiyegemeza na kiSwahili Sanifu au kiIngereza pekee, ambazo ni lugha rasmi Kenya, Timu hii iliyona bora itumiye 'karata' ya lugha asiliya za jamii za Mambasa Mpya kujinasibisha nazo na hivo kuwashawishi wapigaji kura kumṯeuwa kiyongozi wao. Kuṯokana na kwamba ni mkakati mpya na umetumiwa kiubunifu basi sisi t$^{h}$waoneleya ni uvumbuzi.

Kosha moja au mawili, pengine ni kughafilika, au kama nlivosema kwengine Karama (2022), pengine Timu hii ilichukuliya kwamba maaḏamu washaweka miito ya kiSwahili Sanifu, basi ishaṯosheleza kuzijumuisha lugha asiliya za wakaaji wengine wa Mambasa, kwa mfano: kiHinḏi, kiArabu, kiSomali au nrani zaiḏi kiMviṯa, kiBajuni. Lugha hizi zina mifumo yake ya uwanḏḏishi k.m عبد الشعب(kiṯamkoanḏḏishi *eabd alshaeb*), जनता का सेवक (*janata ka sevak*), *u adeega dadka*, متمو ووت, ڤڤچ نچمو kwa maana ya 'mt$^{h}$umwa wa watu'; na رجل للناس (*rajul lilnaas*), लोगों का आदमी (*logon ka aadamee*), *nin dadka* , مت ووت , ڤڤچ نچ 'mt$^{h}$u wa wat$^{h}$u' kwa kiArabu, kiHinḏi, kiSomali, na kiSwahili asiliya (hati ya Swarabic) kwa mṯawaliya huwo. Fasiri hizo nimezipata kuṯoka Google Translate. Au, kwa kuwapa dhana njema, labḏa waliyona lugha hizi zina mifumo ṯafauṯi ya uwanḏḏishi nriposana wakatumiya hati za kiLatini moja kwa moja. Au, pengine miito ya lugha hizi ilitumika kwengine lakini uvinjari wangu haukuziḏirika huku Kisauni. Kosha lengine ni 'asanṯa' waloiṯowa Timu, baaḏa ya kiyongozi wao kuchaguliwa, ilikuwa kwa kiSwahili Sanifu na kiIngereza filhali lugha hizi tulizoshughulikiya zinazo msamiyati wa 'shukurani'. Hili laeleweka na wala Timu hailaumiki. Ni kuwakumbusha ṯu kuwa Mambasa ina jamii nyingi na hivo lugha nyingi ambazo zafaa zijumuishwe kila wakaṯi. Kuhusu masiyala ya 'mt$^{h}$umwa' na 'mtumishi' hayo yaṯaka ḏarasa nzima; tuyawekee siku nyenginee.

Kuṯokana na uvinjari na uchanganuzi wa kijuujuu wenye kumili kwenye data kidogo na iso kina kuhusu miito hii, tunahiṯimisha kuwa uvumbuzi katika kila kadhiya ni jambo ambalo lafaa kuigwa, si katika ch$^{h}$aguzi ṯu, lakini piya katika miito yoyoṯ$^{h}$e ya kimaenreleyo vijijini, mijini, na nchini. Lengo haswa la makala haya, kama anwani yet$^{h}$u inavosema, ni kuṯaka ubunifu na uvumbuzi wa miito hii ya kijumuishi iliyozuliwa wakaṯi wa uchaguzi uliyokwisha majuzi, iipe Uwongozi (wa ASN na Mawaziri wake) unaotekeleza mikakati ya mujukumu katika Mambasa, funzo la kuvumbuwa mikakati mipya ya kwenreleza Mambasa kwenye ufanisi enrelevu.

Nimeambatisha picha hizi kwa niya ya uhifadhi kwa sababu hazikuwamo mitanraoni – si intaneti wala jihazi za kijamii nilizoṯembeleya wakaṯi wa kwanḏḏika makala haya.


KIPNGENO BII
UDA
MALIT RAA
Vote
MALIT
MEMBER OF COUNTY ASSEMBLY
KABIANGA/CHEMAMUL
WARD
CHAGUA ROHO SAFI


ENG. KIPLANGAT JOSPHAT
ENG. KIPLANGAT JOSPHAT
ENG. KIPLANGAT JOSPHAT
MP
BELGUT
2022
MP
BELGUT
2022
MP
BELGUT
2022
UDA
UDA
UDA
#TSUNAMI WA MAENDELEO
#TSUNAMI WA MAENDELEO
#TSUNAMI WA MAENDELEO


THE ORANGE DEMOCRATIC MOVEMENT
Shariff 2022
GOVERNOR Nassir
Omonto Bwa Abanto


THE ORANGE DEMOCRATIC MOVEMENT
Shariff 2022
GOVERNOR Nassir
Omurumikhi wa Bantu


Shariff 2022
Nassir
Mutugati wa Adu


THE ORANGE DEMOCRATIC MOVEMENT
Shariff 2022
GOVERNOR Nassir
Chitab biik


Shariff 2022
GOVERNOR Nassir
The People's Project


Shariff 2022
GOVERNOR Nassir
Mtu wa Watu



Shariff 2022
GOVERNOR Nassir
Jatij Jopiny


Shariff 2022
GOVERNOR Nassir
Mtumishi wa Atu


THE ORANGE DEMOCRATIC MOVEMENT
Shariff 2022
GOVERNOR Nassir
Muthukumi Wenyu






Samahani picha zenyewe hazipenḏezi lakini ni ukusanyaji wa data ghafi nyanjani imebiḏi tuzitumiye hizo hizo. Picha za mwanzo ni zile tulizopiga huku Kabianga, Kericho kabla ya kura za mchujo. Halafu ni picha za kampeni ya Timu. Picha ya pili kuṯoka mwisho ina upanre mmoja wa barabara ya Kisauni, Mambasa. Picha ya mwisho nriyo bango lililoko makutano ya Kengeleni, Mambasa baada ya mgombeya wa Timu kuchaguliwa Gavana na shukurani yao.

**Kongole:** Nawashukuru wanaCHAKIKA na Dkt. Alexander Roṯich wa UoK, kwa kunifaa katika uwaṉḏishi wa makala haya.

**Dhamana:** Maelezo yaliyomo humu ni yangu na si ya UoK, Iḏara yetʰu wala CHAKIKA. Kwa loloṯʰe kuhusu makala haya na Elimu kwa jumla wasiliyana nami mkarama@kabianga.ac.ke .